# Mwongozo wa Jamii Kuhusu Sera ya Mfuko wa Kimataifa wa Uendelevu, Mpito na Ushirikishaji katika Ufadhili

eannaso

Regional Platform
for Communication and Coordination
on HIV/AIDS, Tuberculosis and Malaria
For Anglophone Africa

# Kabla hatujaanza…



## UENDELEVU ina maanisha

*Kuhakikisha kwamba mipango inaweza kuendelea kama inavyohitajika*, ikiwa na fedha za kutosha za misaada na rasilimali watu, na bila mabadiliko katika ubora ama utoaji, tishio kwa haki za kibinadau, ama kumwacha mtu yeyote nyuma.

## MPITO ni:



*Pale nchi inapokuwa haistahili fedha nyengine za mfuko wa kimataifa,* na mipango itatoka kutoka msaada wa Mfuko wa Kimataifa hadi utegemezi wa ndani. Mfuko wa Kimataifa inaelezea mpito kama mkakati wa nchi, ama sehemu ya mpango wa nchi, unaoelekea katika ufadhili na utekelezaji wa mipango yake ya afya bila usaidizi wa Mfuko wa Kimataifa.



## USHIRIKISHAJI KAT

*Mpango ambao Mfuko wa Kimataifa unahitaji nchi kuchangia kiwango fulani wa ufadhili wa ndani ili kugawana gharama za mipango ya Ukimwi,* Kifua Kikuu na malaria na kukuza ufadhili wa kina wa kijinsia kwajili ya matibabu. Kiwango cha fedha ambacho nchi lazima zitoe kwajili ya kupata fedha za Mfuko wa Kimataifa ni tofauti kulingana na uwezo wa nchi husika kulipa.

## KWANINI SERA YA UENDELEVU, MPITO NA USHIKISHAJI KATIKA UFADHILI (STC)?

Katika miaka ya karibuni, wadau wengi – ikiwa ni pamoja na mashirika mengi ya kiraia, mashirika pamoja na makundi ya kijamii – yamehimiza Mfuko wa Kimataifa kuandaa sera ya wazi zitakazo angalia utoaji kwa nchi ambazo hazistahili tena ufadhili. Kuna mifano kadhaa ya mpito ambayo haijakwenda vizuri na zimetishia afya na haki za watu maalum na walio athirika.

**MFANO WA KWANZA:** Kulikua na ongozeko la maambukizi ya Ukimwi miongoni wa watu wanaotumia dawa nchini Romania baada ya Mfuko wa Kimataifa kuondoka mwaka 2010. Mwaka 2013, asilimia 30% ya kesi mpya za Ukimwi zilihusishwa na utumiaji wa dawa ya kudunga ukilinganisha na asilimia 3% mwaka 2010.

**MFANO WA PILI:** Katika eneo la Kaskazini la Mexico (ambapo utumiaji wa dawa ya kudunga ni hatarishi kwa Ukimwi), usambazaji wa sindano ulishuka kwa hadi asilimia 90% kufuatia kutoka kwa Mfuko wa Kimataifa mwaka 2013.

**MUHIMU KWETU WOTE**! Mpito unaweza tishia uendelezi wa utoaji wa huduma muhimu za afya kwa watu maalum na walio athirika. Serikali mara nyingi zina wasiwasi na mipango jumuishi kwajili ya makundi yaliyopigwa marufuku na yale waliyotengwa. Mashirika ya kiraia na makundi ya kijamii LAZIMA yahakikishe kwamba watu maalu na walio athirika hayaachwi nyuma wakati nchi zinatoka katika msaada wa Mfuko wa Kimataifa. Tunaweza fanya hizi kwa kuhimiza serikali, sekta binafsi, na wafadhili wengine kufadhili mashirika na jamii ambazo zinatoa huduma kwa watu maalum na walio athirika.



*Sera ya Mfuko wa Kimataifa wa Uendelevu, Mpito na Ushirikishaji katika ufadhili:*

- Ukuaji wa uchumi haumaanishi kwamba watu wote katika nchi wanapata huduma za afya na kimatibabu.
- Kutokua na usawa ni suala kubwa sana katika nchi zenye uchumi wa kati.
- Kuna masuala ya kutiokua na usawa katika mwito wa watu maalum na walio athirika ambao wanataabika na magonjwa haya matatu, hususan pale kuna sheria ya marufuku, unyanyapaa na ubaguzi.



## *Kanuni za Uendelevu, Mpito na Ushirikshaji katika ufadhili*

Kuna nchi kadhaa za Afrika ambazo zimeainishwa kama nchi za Juu zenye Kipato cha Kati (UMI), kama Afrika Kusini, Angola, Botswana, Gabon na Mauritius. Ingawa ni tajiri ukilinganisha na nyengine, bado kuna kiwango kikubwa cha kutokua na usawa jambo ambalo linaweza hatarisha waathirika kama mpito hautazingatiwa.

*Je mashirika ya kiraia na makundi ya kijamii yanaongea kuhusu uendelevu na mpito katika nchi za Afrika za UMI? Je tunapaswa?*

## KATIKA MKAKATI WA 2017-2011, MFUKO WA KIMATAIFA UNAJIZATITI "KUSAIDIA MWITO WA KIENDELEVU KWAJILI YA KUDHIBITI NA KUHAKISHA MPITO SALAMA."

*Kanuni za Sera ya Mfuko wa Kimataifa wa Uendelevu, Mpito na Ushirikishaji katika Ufadhili (na inamaanisha nini kwetu)!*

| | KANUNI ZA MAZINGIRA MAGUMU YA KIUENDESHAJI (COE) | INAMAANISHA NINI |
|---|---|---|
|  | UTOFAUTISHAJI | Hii inamaanisha kwamba sera ya Uendelevu, Mpito na Ushirikaji katika Ufadhili (STU) pamoja na michakato yake lazima itengenezwe katika kiwango cha mapato ya nchi, muktadha wa ugonjwa, mzigo wa ugonjwa, haki za binadamu na muktandha wa kijinsia, pamoja na masuala mengine ya kimuktadha.<br><br>*Kwanini ina maana kwetu!*<br>Kama mashirika ya kiraia na makundi ya kijamii, kuna fursa za utetezi kwetu ili kuhakisha Mfuko wa Kimataifa unazingatia sera za STC vizuri, katika muktadha mzuri ambao unalinda haki za binadamu na usawa wa kijinsia! |
|  | ULINGANISHI | Hii ina maanisha kwamba mahitaji yanayohusiana na uendelevu na mpito uunganishwe na mifumo ya kitaifa iliyopo na/ama michakato.<br><br>*Kwanini ina maana kwetu!*<br>Lazima tuhakikishe kwamba mtazamo wa uendelevu na mpito ipo katika Mpango wa Mkakati wa Taifa (NSPs) kwajili ya Ukimwi, Kifua Kikuu na malaria. Lazima tushiriki katika uundwaji wa NSPs na kuhimiza kwa lugha hii katika maamuzi! |
|  | UTABIRI | Hii ina maanisha kwamba nchi zinabidi kuwa na notisi ya mapema ili ziweze kijiandaa na mipango ya mpito, ikiwa ni pamoja na kupata rasilimali kwajili ya mchakato.<br><br>*Kwanini ina maana kwetu!*<br>Tunajukumu la kukusanya rasilimali kwajili ya mpito!<br><br>**JE WAJUA? Kitengo cha Community Rights and Gender (CRG) katika Mfuko wa Kimataifa imeweka fedha maalum kwajili ya usimamizi kwa kitaalamu kwenye masuala ya uendelevu na mpito.** |
|  | UWEZO WA KUCHAGUA | Hii ina maanisha kwamba nchi na Mfuko wa Kimataifa zinakubaliwa kuchuka vipengele fulani ya sera hii ili kukidhi muktadha wao,<br><br>*Kwa nini ina maana kwetu!*<br>Kama unadhani kuna masuala ya uendelevu nchini kwako, una jukumu la kutetea ili uhakikishe Mfuko wa Kimataifa Unakidhi matakwa ya sera ya STC. Omba msaada wa kiufundi ama andaa watu/eneo lako kwajili ya ushauri kuhusu uendelevu. Kanuni ya uwezo wa kuchagua ina maanisha una uwezo wa kufanya maamuzi. |

# *Mpango wa Mfuko wa Kimataifa katika Mpito ni upi?*

Ufadhili wa Mipango ya Mfuko wa Kimtaifa ▶ Motisha za ufadhili wa ndani ▶ Weka mipango muhimu kama vile mipango ya watu maalum na walio athirika



## MUHIMU KWETU!

Tathmini ya utayari wa mpito lazima iwe ni jumuishi (ikiwa ni pamjoa na watu maalum na walio athirika), ikizingatia wadau wote, na michakato ya nchi pamoja na jamii na mashirika ya kiraia, ikiongozwa na CCM ama chombo cha uratibu cha wadau. Lengo la tathmini ya mpito ni kuwa kama chombo cha kuchochea mazungumzo katika ngazi ya taifa katika masuala ya mpito katika mitazamo ya kimpango na kifedha. Hakikisha unashiriki!

## MAELEZO YA JUMLA YA SERA YA UENDELEVU, MPITO NA USHIRIKISHAJI KATIKA UDHAFILI WA MFUKO WA KIMATAIFA

| LIC/LMIC | LMIC/U-LMIC | U-LMIC/UMI |
|---|---|---|
| **Nchi zenye kipato cha chini/ Nchi zenye kipato cha kati** | **Nchi zenye kipato cha kati/ Nchi za Juu zenye kipato kidogo cha kati** | **Nchi za Juu-zenye kipato kidogo cha kati** |
| Kusaidia Mpango wa Mkakati wa Taifa (NSPs) kuhakikisha uendelevu wa mipango ya Ukimwi, Kifua Kikuu na malaria<br><br>Kusaidia kuunda Mikakati ya Ufadhili ya Afya katika nchi zilizo na mzigo wa magonjwa na/ama mapato madogo | • Tathmini wa Utayari wa Mpito--;<br>▼<br>• Mpango wa Mpito<br>▼<br>• Mpango wa Mpito kama msingi wa maombi ya fedha inatoka mgao wa nchi | Pale kitengo cha nchi kinakosa ufadhili, kinaweza kupata msaada wa fedha kwa miaka mitatu ya mpito |

**KUELEKEA KATIKA MIPANGO ENDELEVU NA HATIMAYE MPITO**

▶ ▶ ▶

**NCHI ZOTE ZIKIWA KATIKA MPANGO WA USHIRIKISHAJI KATIKA UFADHILI**

## MUHIMU KWETU!

Kuna sheria maalum za ushirikishaji katika ufadhili ambazo zinahitaji serikali kuweka fedha kwajili ya watu maalum na walio athirika

# *USHIRIKISHAJI KATIKA UFADHILI UNAFANYAJE KAZI?*

Mahitaji katika Ushirikishaji katika ufadhili yanafanya vitu viwili vikuu. Yanafanya kazi kuimarisha ufadhili mzima wa sekta ya afya na uendelevu wa mipango ya Ukimwi, Kifua Kikuu na/ama malaria. Mahitaji muhimu ya Ushirikishaji katika Ufadhili:

1. Kuhimiza matumizi makubwa ya serikali katika sekta ya afya ili kufikia malengo ya kitaifa ya upatikanaji wa matibabu kwa wote (UHC); na
2. Kuhakikisha kuna ongezeko la viwango vya ushirikishaji katika ufadhili wa mipango inayosimamiwa na Mfuko wa Kimataifa katika kila kipindi cha mgao, ikilenga kuchukua gharama kuu za mipango ya kitaifa ya magonjwa (Mpango wa Mkakati wa Taifa). Hii ina maanisha kwamba serikali zinapaswa kuahidi fedha nyingi katika mipango inayosaidiwa na Mfuko wa Kimataifa kila mara.

## WASILIANA NA MPANGO WA KIKANDA

Regional Platform for Communication and Coordination for Anglophone Africa Hosted by EANNASOArusha, TanzaniaTel: +255 737 210598Email: eannaso@eannaso.org | Website: www.eannaso.org
Facebook: www.facebook.com/eannaso.org | Twitter: @eannaso